

## MSIJISUMBUE Kwa Neno Lolote

"Msijisumbue kwa neno lolote; bali katika kila neno kwa kusali na kuomba, pamoja na kushukuru, haja zenu na zijulikane na Mungu" Wafilipi 4:6.

Juma lililopita tulikuwa na masomo adhmu. Masomo yalikuwa ni yale ambayo tuliyahitaji kusikia katika nyakati za mateso yetu na majaribu. Ndugu yetu katika Bwana, Sam Willcut alifundisha somo lenye kichwa habari "Msijisumbue kwa neno lolote" ambapo aliwatia moyo wakristo waliokuwa wanateseka katika safari yao kumbebesha Bwana fadhaa zote, 1 Petero 5:7. Na ndugu Willcut aliandika hili kwamba ni "jambo rahisi kusemwa kuliko kutendwa." Ukweli ni kwamba wale walio wana wa Mungu, wana manufaa makubwa kuliko walio nje ya Kristo, yaani tunaye Mungu aliye hai, atoaye, mwenye upendo, atuvishaye na ajuaye haja zetu, Mathayo 6:25-32.

Ingawa twaweza kuelewa jinsi ilivyo rahisi kuwa na wasiwasi na kumezwa na kujisumbua hata kufika hatua ya kulemewa na mashaka, mahangaiko na mawazo. Ingawaje twaweza kujua vilivyo kile ambacho Luka alimaanisha alipoandika kuhusu Martha akisema, "unasumbuka na kufadhaikaka kwa ajili ya vitu vingi" Luka 10:41. Hakuna sababu yoyote kwa mwana wa Mungu leo kuwa hivi, kwa sababu kama vile Paulo alivyosema "Mungu akiwapo upande wetu, ni nani aliye juu yetu?. Unaamini hilo? Basi hujachelewa kuongezea utatuzi mwingine katika maisha yako kwa mwaka 2015. Tatua kwa kumtwika yeye fadhaa zetu zote, kwa sababu:

1. Mungu yu hai (Math. 6:25).
2. Mungu hutoa (Math. 6:26).
3. Mungu ana upendo (Math. 6:26).
4. Mungu hutuvika (Math. 6:28-30).
5. Mungu anazijua haja zetu (Math 6:31-32.)

Ndg. Willcut.

"Msijisumbue kwa neno lolote."